ADVANCE CARE DIRECTIVE.

SWAHILI

Government of South Australia

Advance Care Directive

# Taarifa ya Maelezo

Shahidi wako atakuuliza wewe kusoma hii Taarifa ya Habari, na kisha kukuuliza maswali kadhaa ili kuhakikisha kuwa umeelewa ni nini unafanya kwa kufanya Advance Care Directive.

## Nini maana ya Advance Care Directive?

An Advance Care Directive ni fomu ya kisheria ambayo inawaruhusu watu wenye miaka zaidi ya 18 ku:

- kuandika matakwa yao, upendeleo na maelekezo kwa ajili ya huduma za afya za baadaye, mwisho wa maisha, mipango ya kuishi na mambo ya kibinafsi na / au
- kuteua mtu moja au zaidi wa Kufanya Maauzi -Mbadala ili kufanya maamuzi haya kwa niaba yao wakati wao hawawezi kufanya hivyo wao wenyewe. Haiwezi kutumika kwa ajiri ya kufanya maamuzi ya kifedha.

Kama umeandika kukataa kwa ajiri ya huduma za afya, ni lazima kufuatwa kama inastahili kwa hali ya wakati huo. Taarifa zingine zozote zilizoandikwa katika Advance Care Directive yako ni ushauri na inapaswa kutumika kama mwongozo wa utoaji wa maamuzi na Mtoa Maamuzi-Mbadala wako, wauguzi wa afya yako au mtu mwingine yeyote anayefanya maamuzi kwa niaba yako..

Ni uamuzi wako kama unataka kuwa Advance Care Directive au la. Hakuna mtu anayeweza kukulazimisha kuwa nayo au kuandika mambo siyoyapenda. Haya ni makosa chini ya sheria.

Unaweza kubadilisha Advance Care Directive yako wakati wowote wakati bado ukiwa na uwezo wa kujaza fomu mpya Advance Care Directive yako.

Fomu yako mpya ya Advance Care Directive itakuwa mbadala wa hati nyinginezo zote ulizowahi kujaza unaweza hapo awali, kwa mfano Kutoa Uwezo kwa Mlezi, Uwezo wa Matibabu wa Mwanasheria au Mwelekeo Unaotarajiwa.

## Itatumika lini?

Advance Care Directive yako itatumika tu (inaweza kutumika tu) kama hauwezi kufanya maamuzi yako mwenyewe, yawe ya mda mfupi au ya kudumu.

Kama hauwezi kuelewa:

- kuelewa taarifa kuhusu uamuzi
- kuelewa na kufahamu hatari na faida ya uamuzi
- kukumbuka habari kwa muda mfupi; na
- kumwambia mtu uamuzi ni upi na kwa nini wamefanya uamuzi.

Ina maana kuwa hauwezi kufanya uamuzi (wakati mwingine huitwa kuharibika kwa uwezo wa kuamua) na mtu mwingine atatakiwa kufanya uamuzi kwa ajili yenu.

Advance Care Directive

# Taarifa ya Maelezo

## Nani atafanya maamuzi kwa niaba yako wakati huwezi?

Ni uamuzi wako kuchagua mtu mmoja au zaidi Mbadala wa kufanya maamuzi. Kama umechagua mtu mmoja au zaidi wa Mbadala kufanya maamuzi, watakuwa kisheria kuwezo kufanya maamuzi kwa ajili yenu kuhusu huduma za afya yako, mipango ya kuishi na masuala mengine binafsi wakati unaweza kufanya hivo. Unaweza kutaja aina ya maamuzi unayotaka wao kuyafanya katika Masharti ya Uteuzi ya Sehemu 2b ya Advance Care Directive yako.

Kama usipoteua mtu Mbadala wa kufanya Maamuzi watu wengine wa karibu yako wanaweza kuulizwa kufanya maamuzi kwa ajili yako, ikiwa wewe huwezi (mtu anayehusika). Ni lazima wafuate matakwa muhimu au maelekezo uliyoandika katika Advance Care Directive yako.

Mtu yeyote anayefanya maamuzi kwa niaba yako anahitaji kufanya uamuzi wanaofikiri ungeweza kuyafanya katika hali hiyo hiyo.

## Kukataa huduma ya afya

Unaweza kuwa umeandika katika Advance Care Directive yako kwamba hautaki baadhi ya aina ya huduma za afya, pia inajulikana kama kukataa huduma za afya. Ni muhimu kuhakikisha kuwa umeandika wakati au mazingira gani ukataaji wa huduma za afya utatumika.

Kama umekataa huduma za afya fulani katika Advance Care Directive yako, mtu wa Kufanya Maamuzi wako Mbadala (mtu anayewajibika) na daktari wako wa afya lazima afuate kukataa kwako kama ni muhimu kwa hali yako ya sasa.

Hii ina maana kwamba daktari wako wa afya hataweza kutoa matibabu ya huduma za afya ambayo umeyakataa.

Kama umekataa huduma za afya lakini hujaandika chini wakati gani kukataa kutatumika, kutatumika wakati wote.

Mhudumu wa afya anaweza tu kupuuza kukataa kwa huduma za afya kama kuna ushahidi mkubwa wa kupendekeza kuwa umebadili akili yako lakini hakuwa na Advance Care Directive yako ya sasa, au mhudumu wa afya anaamini kuwa hakuwa na nia ya kukataa huduma za afya kutumika katika mazingira yako ya sasa.

Kama hali hii ikitokea itahitaji idhini kutoka Mfanya Maamuzi Mbadala wako, kama una yoyote, au mtu anayewajibika, kutoa huduma za afya yoyote.

Huwezi kukataa matibabu ya lazima ya afya ya akili kama yalivyotajwa katika jamii au matibabu ya hiari ili kama una yoyote..

## Habari zaidi

Kama ungependa maelezo zaidi tafadhali soma mwongozo wa Advance Care Directive uliotolewa na fomu hii au kwenye mtandao kwenye www.advancecaredirectives.sa.gov.au